1. BIBLIA: UJUMBE WA MUNGU KWA MWANADAMU

“Neno lako ndio kweli”

Shabaha

Ni kuonyesha kwamba Biblia ni neno la Mungu.

Muhtasari

Biblia ni muujiza uliomo katika mikono yetu. Ni kitabu kinakuelezea habali za mabo yaliyo pita bali pia kina kinaunabii mwingi sana, ikiwa na maana kwamba kinatuambia mambo yajayo,mambo ambayo vitabu vingine vyote haviwezi kutujulisha.Kina tufundisha yale yote yaliyo muhimu kwetu kuyajua kuhusu Mungu, mambo yake ambayo Mungu aliyafanya wakati uliopita,anafanya nini kwa wakati huu na kwa wakati ujao amekusudia kufanya nini. Biblia pia hutuonyesha namna itupavyo kuishi ili kumpendeza Mungu.2Timotheo 3:14-17, 2Petro 1:19-21.

BIBLIA

Neno**“Biblia”**maana yake ni**“kitabu”**.Neno**“takatifu”**maana yake**“tenga”**au**“weka kando”.**Kwa hiyo Biblia takatifu ni kitabu kilichotengwa kutoka vitabu vingine.Mungu amekitenga kuwa kitabu pekee kinacho eleza Kweli kuhusu Mungu na mipango yake kwa wanadamu.Tunapoifungua ni kweli kuwa ni mkusanyiko wa vitabu sitini na sita vilivyounganishwa kuwa kitabu kimoja. Biblia imegawanyika sehemu mbili. Agano la kale na Agano jipya.

Agano la kale lina vitabu 39. Musa ndiye mtu wa kwanza kuandika vitabu vitano yapata kama miaka 1500 kabla ya Kristo kuzaliwa.Kitabu cha mwisho kati ya vitabu vya Agano la Kale kiliandikwa na nabii Malaki yapata kama miaka 1000 baadaye.

Agano Jipya lina Vitabu 27. Lina tueleza kuhusu maisha na kazi za Yesu Kristo na jinsi wanafunzi wake walivyoeneza habari njema kuhusu Yesu Kristo na Kuja kwa fufalme wake duniani kote. Sehemu hii ya Biblia iliandikwa wakati wa Mwanzo wa miaka miamoja baada ya Yesu kuzaliwa. Jifunze majina ya vitabu vya Biblia kwa moyo. Itakusaidia katika kusoma na kujifunza kwako Biblia kila siku. Tumeona kwamba Biblia iliandikwa zaidi ya miaka mingi, yapata kama miaka 1600 katika kukamilisha kwake; na bado waandishi wote wanaeleza habari za aina moja zinazo pendeza na kustaabisha. Wanatujulisha kwa namna iliyotofauti, makusudi makubwa kwa ajili ya dunia hii na kwa ajili ya mwanadamu anayekaa juu yake.

Agano la kale lina vitabu 39. Musa ndiye mtu wa kwanza kuandika vitabu vitano yapata kama miaka 1500 kabla ya Kristo kuzaliwa.Kitabu cha mwisho kati ya vitabu vya Agano la Kale kiliandikwa na nabii Malaki yapata kama miaka 1000 baadaye.

Agano Jipya lina Vitabu 27. Lina tueleza kuhusu maisha na kazi za Yesu Kristo na jinsi wanafunzi wake walivyoeneza habari njema kuhusu Yesu Kristo na Kuja kwa fufalme wake duniani kote. Sehemu hii ya Biblia iliandikwa wakati wa Mwanzo wa miaka miamoja baada ya Yesu kuzaliwa. Jifunze majina ya vitabu vya Biblia kwa moyo. Itakusaidia katika kusoma na kujifunza kwako Biblia kila siku. Tumeona kwamba Biblia iliandikwa zaidi ya miaka mingi, yapata kama miaka 1600 katika kukamilisha kwake; na bado waandishi wote wanaeleza habari za aina moja zinazo pendeza na kustaabisha. Wanatujulisha kwa namna iliyotofauti, makusudi makubwa kwa ajili ya dunia hii na kwa ajili ya mwanadamu anayekaa juu yake.

JINSI BIBLIA ILIVYOANDIKWA

Ni kwa jinsi gani Biblia, ambayo iliandikwa zaidi ya kipindi cha muda mrefu sana tena kwa kuandikwa na watu wengi tofauti na walioishi sehemu tofauti, wote waelezee ujumbe mhimu wa aina moja? Mtume Petro anatuambia kwamba:**“Watu wa Mungu walinena wakiongozwa na Roho Mtakatifu”**(2Petro 1:21).Ilikuwa ni nguvu takatifu za Mungu iliyowapatia watu hao fikra katika mawazo yao nao wakayanena yale ambayo ni mawazo ya Mungu, kwa hiyo, ingawaje watu wengi waliandika Biblia, lakini Mungu mwenyewe ndiye mtungaji wa Biblia.

.

KWA NINI BIBLIA ILIANDIKWA.

Katika Biblia tunaambiwa yote ambayo ni ya muhimu kwetu kuhusu Mungu na mpango wake kwa dunia na wanadamu wanaokaa juu yake.Mungu anataka sisi tumjue na tumpende Yeye. Kuna aina nyingi ya habari nzuri zinazovutia na kufurahisha katika Biblia kuhusu wanaume na wanawake waaminifu waliompenda na kumtii Mungu.Habari hizi zinatusaidia sisi kujifunza kuwa waaminifu na watiifu pia. Kwa hiyo kwa kadri tunavyosoma Biblia, na ndivyo kadri tunavyompenda Mungu na kujaribu kumpendeza Yeye. Na nia zetu zitaweza kuwa nia yake Mungu na njia zetu zitabadilishwa kufunana na njia zake.

KUSUDI LA MUNGU LA WAKATI UJAO KWA DUNIA.

Kusudi la Mungu ni kuijaza dunia utukufu wake Mungu.**"Hakika kama niishivo,dunia yote itajazwa na utukufu wa Mungu"**(Hesabu 14:21).Ilikufanya hili atamtuma Yesu Kristo kurudi hapa duniani kuuweka ufalme wa Mungu hapa duniani (Matendo 1:10 – 11, Dan 2:44). Kwanza atawafufua wafu wale waliojua kweli na atawapatia wote uzima wa milele waliompenda na kumtii. Kisha watamsaidia kuifundisha dunia njia ya haki ya Mungu. Atawaangamiza wabaya na kutawala katika Yerusalemuakiwa Mfalme wa dunia yote. Kisha kwa miaka elfu moja Kristo na watakatifu wake wataibadilisha dunia kuwa mahali ambapo viumbe vyote vitampatia Mungu utukufu na sifa milele.

YANAYOFUNDISHWA NA BIBLIA KUHUSU MUNGU.

Biblia inatuambia kuwa Mungu:-

1. Kwamba Mungu ni Roho au kamwe Yeye hafi
2. Kwamba kuna Mungu mmoja (Kumb. 6:4), Muumbaji wa vitu vyote.
3. Kuwa Mungu ni mwema na mvumilivu na huwa saidia na kuwaongoza wale wanaomwanini yeye. Pia yeye ni mwenye haki na mwaminifu atawahukumu waovu waliomkataa Yeye pamoja na njia zake.
4. Kuwa Roho Mtakatifu nguvu za Mungu ambayo kwa njia yake Mungu hutenda matendo yake makuu na ya ajabu.
5. Kwamba malaika ni watumwa wake wa kiroho au wajumbe wake watendao mapenzi yake.

FUNDISHO

Katika Biblia tunajifunza yale ambayo Mungu anataka sisi tuyafanye. Kuna ambo ambayo tunapaswa kuyafanya na mambo yale ambayo hatutakiwi kuyafanya. Wale watu wanaofanya yale Mungu anayoyataka kwa sababu wanampenda na kumwamini, siku moja watapewa uzima wa milele katika ufalme wa Mungu. Hakuna sehemu nyingine isipokuwa katika Biblia ndipo tunakuta njia ya uzima wa milele na furaha tele. Tunatakiwa tusome biblia kila siku naye Mungu atatuongoza katika maisha yetu yote.**"Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu"**(Zaburi 119:105)

MAELEZO YA NYONGEZA

Unabii ni nini?Wakati ambapo watakatifu wa Mungu walipotabiri, walinena habari ya mambo yajayo.Kwa mawazo yetu sisi hatuwezi kuyasema yale yatakayotokea wakati ujao ila Mungu ndiye anaweza kusema yatakayotokea wakati ujao. Biblia ina mkusanyiko mwingi sana wa unabii. Zingine zimekwisha kutimia kwa kila namna ya maelezo yaliyokuwa yametabiriwa kiasi ambacho tunakuwa kuamini kwa uhakika kwamba hata unabii mwingi ambao haujatimia bado, utatimizwa kwa kweli hakika. unabii mwingi sana wa Biblia unaonyesha waziwazi kwamba yesu kristo atarudi duniani, na zinaeleza ishara zitakazo kuwepo kabla hajarudi.

Fikiria baadhi ya ishara hizi:

1. Kutakuwepo na dhiki kuu na vita kati ya mataifa ya dunia (Dan 12:1, Luka 21:25 –26.)
2. na dhambi zitaongezeka duniani (Mathayo 24"37 – 39)
3. Watoto hawatawaheshimu wazazi na wakubwa wao,na watu watapenda anasa kuliko kumpenda Mungu(2Timotheo 3:1-5)
4. nchi ya Urusi itakuwa ni nchi yenye nguvu sana na itataka kuitawala dunia(Ezekieli 38)
5. Wayahudi watarudi katika nchi yao wenyewe (Eze 38:8, 12)

Unabii huu unaendelea kutimizwa siku hizi machoni petu wenyewe na huu ni ushuhuda kwamba Biblia ni neno la Mungu hakika, na ya kuwa siku ile ikaribu sana ambapo Mungu atamtuma Yesu Kristo kurudi duniani kuuweka ufalme wa Mungu.

MASWALI

Maisha ni Mafupi

1. Ni nani mwandishi wa Biblia?
2. Biblia Takatifu maana ninini ?
3. Kuna vitabu vingapi katika Biblia?
4. Ni kwa nini Mungu alitaka Biblia iandikwe?
5. Ni nini makusudi ya Mungu kwa dunia?
6. Nini maana ya Roho Mtakatifu?
7. Malaika ni nani?
8. Makusudi ya Mungu kwa wale wampendao ni nini?

Majibu ya Kina

1. Biblia inatufundisha nini kuhusu Mungu?
2. Eleza yale unayoyajua kuhusu mpango Mungu kwa dunia

Majibu ya Nyongeza

1. Biblia ina unabii mwingi sana unaoonyesha kwamba kurudi kwa Yesu Kristo duniani kumekaribia. Baadhi ya unabii huu ni nini?